SHIRIKA LA RELI TANZANIA

RELI na MATUKIO Gazeti

Juni 04, 2021



Gazeti la Reli | Toleo Namba 14 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha


# RAIS SAMIA AIPONGEZA TRC, ATOA 372.34 BILIONI



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa Ikulu jijini Dar es Salaam Mei, 2021.**

Na Mwandishi wetu

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) Masanja Kadogosa kuhusu maendeleo ya miradi ya ujenzi wa reli na maendeleo ya shirika hilo, Mei, 2021

Katika mazungumzo hayo, Kadogosa amemshukuru Mhe. Rais Samia kwa Serikali kuidhinisha Sh 372.34 Bilioni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kipande cha reli ya Mwanza – Isaka chenye urefu wa kilometa 341 kwa kiwango cha kisasa

"Kadogosa ameeleza kuwa tangu Rais Samia aingie madarakani ujenzi wa reli katika vipande viwili unaendelea vizuri ambapo hadi mwezi uliopita kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (kilometa 300) kilikuwa kimefikia asilimia 91 na Morogoro – Makutupora (kilometa 422) kilikuwa kimefikia asilimia 60.02," inaeleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo imebainisha kuwa majaribio ya treni ya abiria yanatarajiwa kuanza mwishoni mwa Agosti, 2021 kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro.

Inaendelea Uk. 2







# RAIS SAMIA AIPONGEZA TRC, ATOA 372.34 BILIONI

Na Mwandishi wetu Inatoka Uk. 1



Mwanza - Isaka ikiendelea Bukwimba mkoani Mwanza Mei, 2021. Mradi wa SGR Mwanza - Isaka utakuwa na Kambi kubwa nne ambazo ni Fela, Bukwimba, Malampaka na Lohumbo.

Kwa upande wake Rais, Mhe. Samia amesema Serikali imedhamiria kuhakikisha ujenzi wa reli ya kati utakaounganisha Bandari ya Dar es Salaam na Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi unakamilishwa ili kuzifikia nchi za Uganda, Burundi, Rwanda na DRC.

Kiongozi mkuu huyo amemtaka Kadogosa kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo ya ujenzi vizuri ikiwa ni pamoja na kujipanga kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutopora – Tabora, Tabora – Isaka na Kaliua – Mpanda – Kalema.

"Rais Samia ameipongeza TRC chini ya Kadogosa pamoja na wote wanaoshiriki katika ujenzi wa reli kwa kazi nzuri wanayoifanya na ameeleza kuridhishwa kwake na maendeleo ya miradi hiyo," inaeleza taarifa hiyo.



Kazi ya ujenzi wa uzio wa reli ya kisasa - SGR Dar es Salaam - Morogoro ikiendelea katika eneo la Mpiji mkoani Pwani ambapo uzio huo unajengwa ili kuzuia Watu na Wanyama kukatiza katika reli hiyo itakayopitisha treni za mwendokasi wa KM 160 kwa saa.

# WAZIRI MKUU ATOA HEKO KWA TRC



Na Mwandishi wetu



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa akimuelezea Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa kuhusu picha ya Mwalimu Julius Nyerere iliyowekwa sehemu ya Mapokezi katika jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam hivi karibuni, 2021.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ametembelea mradi wa ujenzi Reli ya Kisasa (SGR) kukagua jengo la Stesheni na ujenzi wa Daraja linalounganisha Stesheni hiyo ikiwa ni ziara ya kufuatilia miradi mbalimbali ya kimkakati inyoendelea kutekelezwa nchini, Aprili 20, 2021.

Katika ziara hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelipongeza Shirika La Reli Tanzania (TRC) kwa kazi nzuri inayofanywa ya kusimamia mradi na kuwataka wafanyakazi wa shirika hilo kufanya kazi kwa bidii kwa kuwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewahakikishia wananchi kuwa mradi huu na mingine ya kimkakati itaendelea na kukamilishwa kama ilivyopangwa.

“Mradi huu tutaendelea kuujenga hadi uishe, tutaendelea na awamu ya pili (Tabora - Kigoma) na ya tatu (Tabora – Mpanda - Karema)” alisema Waziri Mkuu

Aidha, Mheshimiwa Kassimu Majaliwa ameongeza kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi zipo na serikali imejipanga vizuri, hivyo amelitaka Shirika La Reli Tanzania (TRC) kumsimamia mkandarasi vizuri na kuzitumia fedha hizo vizuri.

“Raisi wetu Mhe. Samia Suluhu Hassan amenihakikishia hela ipo na tumejipanga vizuri na kwa utulivu na amani, Serikali yetu haitabadilika, pesa tulizoziweka kwenye mradi zitatumika vizuri” aliongeza Mhe. Waziri Mkuu.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Dkt. Leonard Chamuriho, alitolea ufafanuzi kuhusu kuchelewa kukamilika kwa mradi kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ni kutokana na kutokukamilika kwa daraja la KM 2.56 linaounganisha Stesheni ya Dar es Salaam kwa lengo la kuepukana na msongamano wa magari na watu katikati ya jiji, hata hivyo Waziri Chamuriho ameeleza kuwa ifikiapo mwezi Agosti treni zitaanza kutembea kuanzia stesheni ya Pugu kuelekea Morogoro.


Katika ziara hiyo Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa alitoa taarifa ya maendeleo ya mradi kuwa kipande cha kwanza kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro kimekamilika kwa 91% ambapo makalavati 248 yameshakamilika kujengwa, madaraja 117 nayo tayari yameshakamilika na matarajio ni kuwa ifikapo Agosti mwaka huu uendeshaji wa treni kutoka Pugu mpaka Morogoro utaanza.

“Mheshimiwa waziri Mkuu, stesheni hii ya Dar Es Salaam imekamilika, kinachoendelea ni uwekaji wa mifumo ya mawasiliano, ulinzi na kusawazisha eneo, utakapo kuja tena utakuta mandhari nzuri sana,mpaka sasa tuna asilimia 91 imekamilika katika ujenzi huu“ Alisema Kadogosa

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa TRC aliongeza kuwa awamu ya pili ya ujenzi wa mradi imekamilika kwa 61.7% kwa wakati huo na mpaka sasa ujenzi wa reli umekamilika kwa zaidi ya asilimia 61 na ifikapo Agosti mwaka huu kipande cha Morogoro - Makutupora kitakuwa kimeunganishwa na kufikia Februari 28, 2022 kipande hiki kitakuwa kimekamilika.

# NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI ARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa akimuonesha Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Mwita Waitara, saini ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alipotembelea Handaki namba 2 la Reli ya SGR Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni, 2021.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Mwita Waitara (kati) akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Kelvin Kimaro (kushoto) katika maabara ya kupima Mataruma katika kambi ndogo ya Mradi wa SGR iliyopo Igandu mkoani Dodoma hivi karibuni, 2021

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Mwita Waitara aridhishwa na maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Morogoro – Makutupora ambao ujenzi wake umefikia 61%, hivi karibuni 2021.

Mhe. Waitara ameyasema hayo alipokuwa katika ziara yake kukagua mradi wa SGR Kilosa mkoani Morogoro, ambapo ziara hiyo ya siku mbili ilihusisha ukaguzi wa Mradi kwa kipande cha Morogoro – Makutupora na Dar es Salaam – Morogoro kwa lengo la kuona mwenendo wa mradi huo.

Mhe. Naibu Waziri ameeleza kuwa ameridhishwa na maendeleo ya mradi huo wa kimkakati kwakuwa kazi zinakwenda vizuri na Watanzania wananufaika na mradi wakati huu wa ujenzi na hata mradi utakapokamilika.

“Leo nimefanya ziara kujiridhisha na kazi inayoendelea katika kipande hiki cha pili cha ujenzi wa reli hii ya kisasa kutoka Dodoma hadi Morogoro, nimeridhishwa kwamba kazi inakwenda vizuri na nimefurahi kwakuwa vijana wetu wazawa wapo kazini wanafanya kazi jambo ambalo litasaidia pindi wakandarasi watakapoondoka tutakuwa na wataalamu watakaosimamia mradi huu” alisema Mhe. Waitara.

Aidha, Mhe. Naibu Waziri amewataka wafanyakazi wazawa wanaoshiriki katika mradi kuwa walinzi wa vifaa na malighafi zinazotumika katika mradi huo, kwakuwa uzalendo na uaminifu wao utaweza kuwanufaisha katika kupata fursa za ajira hapo baadae, pia itasaidia mradi huo kukamilika na hatimaye kuwanufaisha watanzania

“Watanzania mliopata fursa kufanya kazi katika mradi. mna jukumu la kulinda vifaa na mitambo inayofanya kazi hapa, tunaamini kwamba ninyi ni waaminifu na serikali inaamini hivyo” aliongeza Mhe. Waitara

Halikadhalika, Mhe. Naibu Waziri alieleza kuwa “Mradi huu utakapokamilika kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, muonekano wa nchi yetu utabadilika sana, uchumi wetu utakua, tutaongeza watalii wa ndani na nje hivyo nawasihi watanzania waendelee kuwa na imani na Serikali inayoongozwa na Mhe. Samia kuwa Miradi yote ya kimkakati itakamilika”

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa ameshukuru ujio wa Mhe. Naibu Waziri kwa kusema kuwa “Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuona kinachoendelea na kuridhishwa na kazi, sambamba na hayo ametoa maelekezo ambayo ni lazima tuyafanye kwa utiifu na uzalendo”

Kadogosa alisisitiza kuwa mpaka sasa Mradi huo kwa kipande cha Morogoro – Makutupora umeshafikia 61%, ujenzi unaendelea kwa kasi na lengo ni kuunganisha Ihumwa na Pugu ifikapo mwezi Agosti 2021, Kadogosa ameahidi kuwa Shirika litaendelea kusimamia Mradi kwa uzalendo na kwa utii wa serikali na nchi.

# TRC YAENDELEA KUTATUA CHANGAMOTO ZA JAMII KARIBU NA ENEO LA MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la Reli Tanzania – TRC kupitia Wataalamu wake kutoka vitengo mbalimbali kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa mpaka ngazi ya Vijiji wameendesha zoezi la kufanya tathimini za athari na changamoto zilizojitokeza kwa wananchi walio katika maeneo ambayo ujenzi wa reli ya kisasa –SGR unaendelea, Mkoani Morogoro Mei, 2021.

Zoezi lilianzia Mkoani Dar es Salaam, Ilala mpaka Morogoro ambapo lengo kubwa la zoezi hilo ni kupita katika maeneo yote sambamba na kutatua changamoto na malalamiko yote ambayo Shirika la reli lilipokea kutoka kwa wananchi ambao wameathirika na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha kwanza Dar es Salaam – Morogoro.

Aidha, zoezi hilo limejikita hasa katika kutatua changamoto ambazo wananchi zimewapata kutokana na ujenzi wa reli hasa wananchi waishio maeneo hatarishi, wananchi wanaoshindwa kupata huduma za kijamii, kuhakiki wananchi ambao wameshalipwa fidia kama wameachia maeneo na kusikiliza malalamiko ya ardhi na fidia pamoja athari za mazingira wanazokutananazo wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Mhandisi Rajab Mahaja kutoka TRC, ambaye ni kiongozi wa wataalam hao, amaeeleza namna zoezi lilivyoendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu kutatua changamoto za wananchi huku ikionekana kuwa idadi kubwa ya wananchi waliolalamika kutokuridhika na fidia na ardhi ikiwa ni ukosefu wa elimu ya kutosha hasa katika mambo ya ulipaji fidia na utwaaji wa ardhi na mara tu baada ya wananchi kupewa elimu waliridhika na kuona hakuna ambacho wanadai kutoka kwa Shirika la Reli Tanzania.

“Tumefika katika maeneo yote tukafanya tathimini, baadhi ya wananchi waliokuwa wakilalamika na kusema Shirika limewapunja fidia tuliamua kuwapa elimu ya namna zoezi la uthamini linavyofanyika wengi walielewa na baada ya kuoneshwa jedwali la uthamini waliona kabsa hawana ambacho wanadai kwa Shirika” alisema Mhandisi Mahaja.

Hata vivyo Mhandisi Mahaja aliongeza kuwa, elimu waliyoitoa kwa wananchi imeleta manufaa chanya kwao na kwa Serikali kwa ujumla kwa sababu viongozi wa Serikali walio katika maeneo hayoo wamekuwa wakisumbuliwa sana na wananchi kwa madai ya kuwa Shirika halijawapa fidia stahiki. Hivyo kupitia elimu waliyopewa kabla ya kuanza kutatua changamoto wananchi wameweza kuona namna Shirika lilivyofuata Sheria ya ardhi na fidia katika kutwaa maeneo yao.

Katika hatua nyingine, Mhandisi Mahaja ameeleza kuwepo kwa vitendo vya ukaidi kwa baadhi ya wananchi ambao tayari wamekwisha kulipwa fidia lakini bado hawajaondoka na baadhi yao kubomoa nyumba upande mmoja na kuendelea kukaa katika maeneo hayoo na wengine kupangisha hivyoo alitoa wito kwa wale wote wanaoendelea kukaidi watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Naye Bi. Lightness Mngulu Mtaalam wa Masuala ya Kijamii – TRC, amebainisha kuwa zoezi la kupita na kuona changamoto zinazoikumba jamii zinazoishi eneo la mradi ni jambo ambalo limeleta afya kwa jamii husika lakini pia kwa Shirika la Reli, kutokana na kwamba kwa muda mrefu wao kama wataalam wa mambo ya jamii wamekuwa wakipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, hivyo kitendo cha Shirika kujitokeza na kutatua changamoto na zingine kuzipeleka ngazi za juu ni jambo la muhimu kwa jamii na inaonesha uwajibikaji chanya wa Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania .

“Tumekuja kutatua changamoto pamoja na malalamiko yote angalau tuweze kuona namna ya kuweza kuwarudishia maisha yao kama ilivyokuwa awali. Kupitia zoezi hili tutakuwa tumepunguza kwa asilimia kubwa malalamiko ambayo yalitufikia na kuna mengi hayakutufikia wananchi walibaki nayoo na kuendelea kulalamika lakini baada ya kukutana na wananchi wa maeneo haya tumeweza kuyabaini na kuyatafutia ufumbuzi chanya kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewatendea haki wananchi na wataufurahia mradi wao” alisema Bi Lightness.



Mhandisi Rajabu Mahaja akitoa elimu ya uthamini ardhi na malipo ya fidia kwa wananchi wa kata ya Kihonda mkoani Morogoro kabla ya kusikiliza malalamiko na changamoto zao, Mei 2021

# WAFANYAKAZI TRC WAADHIMISHA SIKU YA WAFANYAKAZI MEI MOSI

Na Mwandishi wetu

Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania – TRC washiriki Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi iliyoadhimishwa kitaifa katika viwanja vya CCM Kirumba jijini Mwanza Mei 01, 2021.

Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani hufanyika Mei 01 kila mwaka Duniani kote kwa lengo la kuwakutanisha wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi ambapo kauli mbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka 2021 ni "Maslahi Bora, Mishahara Juu" huku Mgeni Rasmi akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Sambamba na ushiriki wao katika maadhimisho ya kitaifa, wafanyakazi wa TRC katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Dodoma, na Tabora waliadhimisha sherehe hizo kwa kufanya maandamano katika maeneo yao.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amekabidhi Hundi kama zawadi kwa Wafanyakazi Bora na Hodari wa Shirika kwa mwaka 2021, ambapo Mfanyakazi Bora Bwana Mommy Mwakyusa amepata Shilingi Milioni Tatu akifuatiwa na Bwana Bura Maringa aliyepata nafasi ya Mfanyakazi Hodari na kukabidhiwa Shilingi Milioni Mbili huku washindi wengine Sita kutoka Makao Makuu, Kanda ya Dar es Salaam, Tanga na Tabora wakipata ya Shilingi 1,500,000 kila mmoja.

"Leo Mhe. Rais amekabidhi zawadi kwa Wafanyakazi Bora lakini pia sisi tumekutana hapa kama wafanyakazi kupongezana kwa baadhi ya wafanyakazi waliofanya vizuri na nimekabidhi pia zawadi za Shilingi 2,000,000 kwa mfanyakazi Hodari, na Shilingi 1,500,000 kwa wafanyakazi Hodari wengine sita pia tumekutana kujadili Mustakabali wa Shirika letu" alisema Kadogosa

Mkurugenzi Mkuu wa TRC amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhudhuria Sherehe za Mei Mosi na ameongeza kuwa mambo ambayo Mhe. Rais ameyazungumza yamewagusa wafanyakazi wa Shirika hilo ikiwemo kupunguza Kodi katika Makato ya Mishahara na Mikopo ya vyuo vikuu lakini pia ameahidi kuhakikisha Shirika linaongeza tija katika uzalishaji ili kuongeza mapato kama alivyoagiza Mhe. Rais.

Mmoja wa wafanyakazi Bora Bi. Regina Singano ameeleza hisia zake mara baada ya kupokea zawadi yake "Nimefurahi sana kuwa mfanyakazi Hodari namshukuru Mwenyezi Mungu kwani bila yeye, bila wafanyakazi wenzangu nisingeweza kuwa mfanyakazi hodari, naishukuru ofisi yangu nalishukuru Shirika la Reli"

Naye Awadhi Mashanga, Muongoza Treni Mwanza amesema kuwa amefarijika na ameona kuwa taasisi imemtendea haki kwa zawadi iliyompatia lakini pia anatarajia zawadi hizo zitakuwa kama motisha kwa wafanyakazi wengine waweze kuchapa kazi zaidi.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa na baadhi ya Viongozi wa TRAWU wakimpongeza Mfanyakazi Bora wa TRC kwa mwaka 2021 Bwana Momy Mwakyusa wakati wa hafla fupi ya kuwapongeza wafanyakazi bora iliyofanyika City Garden jijini Mwanza Mei 01, 2021.




Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe mbalimbali kwa ajili ya maandamo wakati wa Sherehe za Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi, jijini Mwanza Mei 01, 2021.



Muonekano wa Sehemu wa jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR jijini Dar es Salaam likiwa limekamilika kwa 100%.



Sehemu ya uzio wa Reli ya Kisasa - SGR ulioanza kujengwa Mpiji mkoani Pwani Mei, 2021.





Wahandisi wa Umeme TRC wakiendelea na kazi ya majaribio ya mitambo ya umeme iliyofungwa katika kituo cha umeme wa SGR Kidugalo mkoani Morogoro Mei, 2021.



Moja kati ya vivuko vya reli (Rail over Rail) vitano vilivyojengwa katika mradi wa SGR Dar es Salaam - Morogoro, ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 100.



Muonekano wa Jengo la ofisi ya Makao Makuu ya Shirika la Reli Tanzania - TRC linaloendelea kujengwa katika eneo la Kikuyu kusini jijini Dodoma.



Muonekano wa jengo la Stesheni ya SGR Kilosa mkoani Morogoro ambalo ujenzi wake unaendelea.



Ujenzi wa Daraja linalokatiza mto Mkondoa uliopo Kilosa mkoani Morogoro ukiendelea mkoani Morogoro Mei, 2021.



Ujenzi wa Karakana na sehemu ya Treni za mizigo ukiendelea Kwala mkoani Pwani Mei, 2021.



Stesheni ya abiria na mizigo ya Ruvu ikiwa imekamilika kwa asilimia 100 mkoani Pwani, Mei, 2021.

# TRC YAENDELEA NA ZOEZI LA FIDIA MKOANI MWANZA NA SHINYANGA KUPISHA UJENZI WA KAMBI ZA SGR

Na Mwandishi wetu TRC



Bwana Paschal Thomas, Afisa Ardhi TRC akimsainisha mkazi wa Didia wilaya ya Shinyanga Bi. Monika Shigula kwa ajili ya malipo ya fidia ili kupisha ujenzi wa kambi ya SGR mkoani Shinyanga Mei, 2021.



Matukio tofauti wakati wa zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi wa Didia katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ili kupisha ujenzi wa Kambi ya mradi wa SGR mkoani Shinyanga Mei, 2021.

Shirika la Reli Tanzania – TRC laendelea na zoezi la ulipaji fidia ili kupisha ujenzi wa kambi za Mradi wa reli ya Kisasa – SGR katika maeneo ya Fela, Bukwimba, Malampaka mkoani Mwanza na Didia mkoani Shinyanga Mei, 2021.

Zoezi hilo linaendelea chini ya usimamizi wa Maafisa kutoka TRC wakishirikiana na maafisa kutoka Wilaya husika mkoani Shinyanga na Mwanza ambapo Mei 17, 2021 zoezi limeendeshwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tarafa ya Ikungwi katika kijiji cha Didia ambapo wananchi 20 wamepokea hundi za malipo ya fidia.

Aidha, ulipwaji wa fidia unakwenda sambamba na maandalizi ya uzinduzi rasmi wa Mradi huo kipande cha Mwanza – Isaka chenye urefu wa KM 341, ambapo mara baada ya uzinduzi huo kufanyika hivi karibuni shughuli za ujenzi wa reli ya kisasa zitaanza rasmi na kuwawezesha wananchi kuanza kunufaika na mradi huo.

Mradi wa SGR Mwanza – Isaka unapita katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga ambapo kwa hatua za awali tayari wananchi wa maeneo ya Fela, Didia. Malampaka na Bukwimba ambayo kambi za mradi huo zitajengwa wameendelea kupokea fidia ili kupisha ujenzi wa kambi za mradi huo.

Wananchi wa maeneo hayo ambao wamepatiwa fidia zao wameridhishwa na zoezi hilo ambapo wameeleza kuwa fidia hizo zimelipwa kwa wakati na wamefurahishwa kwa kuwa ahadi iliyotolewa na Serikali kwa kila mwananchi ambaye eneo lake limepitiwa na mradi kulipwa fidia anayostahili imetimizwa.

Mradi wa SGR Mwanza – Isaka unatarajiwa kuzalisha jumla ya ajira za moja kwa moja zaidi ya 11,000 zitazalishwa na zisizo moja kwa moja zaidi ya 55,000 na utachochea ukuaji wa uchumi kwa kuvipatia nafasi viwanda vya ndani fursa ya kuuza malighafi za ujenzi.

# FIDIA, NA KIFUTA MACHOZI KATIKA UJENZI WA SGR NI HAKI YA MSINGI KWA WANANCHI

Na Mwandishi wetu TRC

Tangu mwaka 2017, ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipoamua kuanza kujenga miundombinu ya reli ya kisasa – SGR, Shirika la Reli Tanzania – TRC kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wameendelea kutwaa ardhi ya Mamilioni ya watanzania katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza, wakiwa na lengo la kupisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa nchini.

Kimsingi suala la utwaaji ardhi na fidia katika nchi yetu ni kitu kisichoepukika kwa sasa kulingana na uhitaji mkubwa wa Ardhi kwa miradi yenye manufaa ya umma kwa ajili ya uwekezaji au shughuli yeyote inayofanywa na Serikali, Taasisi au Mamlaka yeyote ya Serikali au binafsi hasa za maendeleo ya taifa.

Katika utekelezaji wa ujenzi wa reli ya kisasa ni dhahiri kwamba maeneo mengi ya wananchi yametwaliwa na Serikali kwa ajili ya kupisha ujenzi wa reli ya kisasa. Shirika la Reli limetwaa ardhi kwa kuzingatia Sheria na kanuni za Ardhi ikiwemo malipo ya fidia na Kifuta machozi ambazo ni haki kwa wahusika.

Mara baada ya Shirika la Reli Tanzania kuamua kutwaa ardhi, hatua inayofuata ni ulipaji wa Fidia kwa wananchi mara baada ya kutwaa rasilimali zao kwa lengo la kupisha ujenzi wa reli ya kisasa – SGR. Zoezi la utwaaji ardhi liko kisheria kwa kuwa malipo hayo hutolewa kwa mtu ama Taasisi kama mbadala wa mali yake kutokana na kuondolewa kwenye eneo lake lililotwaliwa kwa manufaa ya umma na kupangiwa matumizi mengine tofauti nayale yaliyokuwepo.

Hivyo Shirika linapotwaa rasilimali za wananchi pamoja na uhamishaji makaburi kwa lengo la kupisha Shughuli za maendeleo ya Taifa ikiwa ni ujenzi wa SGR hivyo huamua kuwalipa Fidia ama kifuta machozi kama haki ya msingi ya wamiliki hao kulingana na thamani ya ardhi katika eneo husika ambapo Mthamini Mkuu wa Serikali ndiye husimamia kazi ya uthaminishaji wa ardhi na mali za wananchi.

Aidha, Shirika la Reli nchini limeendelea na malipo ya fidia pamoja na kifuta machozi kwa kuhakikisha kwamba wananchi ambao ardhi yao imetwaliwa wanalipwa fidia ambayo ni kamilifu, na haraka na ya haki. Haki katika fidia ya ardhi hutendeka baina ya Shirika pamoja na wamiliki wa ardhi husika, kwa maana ya kwamba mlipaji na mlipwaji wa fidia wote wanahaki sawa, na haki hiyo hupatikana kwa kufanya uthamini wa mali husika kabla fidia haijalipwa.

Maafisa Ardhi kutoka Shirika la Reli wamekuwa wakiendesha zoezi hilo kwa kuzingatia rasilimali iliyo juu ya ardhi au maendeleo yaliyofanyika katika ardhi. Mfano, iwapo kwenye ardhi hiyo kumejengwa nyumba, au kumepandwa mazao basi tathimini hufanyika kwa kuzingatia bei halisi ya soko kama ilivyopitishwa na kutangazwa na mamlaka serikali. Tathimini ikishafanyika malipo hufanyika kwa wakati maalumu ili kuendana na thamani ya mali hiyo.

Katika hatua nyingine, hivi karibuni Shirika la Reli Tanzania limeendesha zoezi la ulipaji wa kifuta machozi kwa wananchi ambao makaburi ya ndugu zao yalihamishwa kwa lengo la kupisha ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha pili Morogoro mpaka Makutupora, Singida.

Zoezi la ulipaji kifuta machozi lilifanyika katika Mkoa wa Morogoro mpaka Mkoani Dodoma na Singida. Malipo hayo ni baada ya Shirika kutwaa ardhi ili kupisha ujenzi wa SGR na kuamua kuhamisha makaburi hayo na kupeleka sehemu husika ambayo serikali ya kijiji ilitenga. Jumla ya makaburi 1,439 yalihamishwa katika vijiji 37, na Serikali kutenga kiasi cha fedha za kitanzania Shilingi 760,703,624.28 kwa ajili ya kuwalipa wananchi hao kama kifuta machozi.

Kwa upande mwingine, mara baada ya zoezi la ulipaji fidia linapokamilika, Shirika huendesha zoezi la kufanya tathimini za athari na changamoto zilizojitokeza kwa wananchi walio katika maeneo ambayo ujenzi wa reli ya kisasa unaendelea. Tathimini hiyo hujikita hasa katika kutatua changamoto ambazo wananchi zimewapata kutokana na ujenzi wa reli kwa kusikiliza malalamiko ya ardhi na malipo ya fidia kwa wale ambao hawakurizika na uthamini wa ardhi na malipo.

Kwa ujumla, fidia haipaswi kumsababishia mhusika ugumu wa maisha ambao hakuwa nao kabla ya kutwaliwa ardhi na mali iliyopo katika ardhi yake, badala yake, fidia inapaswa ijumuishe malipo ya thamani ya ardhi na mali au kifuta machozi cha kumfanya mtu ambaye ameondoka katika eneo analolimiliki ajisikie faraja na kukiri kwamba kuhamishwa kwake kuna manufaa kwake yeye mwenyewe na wananchi wenzake.



**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**
**Barabara ya Sokoine**
**S.L.P 76959**
**Dar es Salaam**
**TANZANIA**
**Barua pepe; info@trc.co.tz**
**Simu ya Bure; 0800 110 042**

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

| | |
|---|---|
| MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk |
| MHARIRI MSAIDIZI | Sami Omary |
| MAKALA | Aziza Charles & Hemed Mohamed |
| HABARI | Amina Juma |
| PICHA | Seleman Kadiko |
| KIBONZO | Hassan Said |
| MTAYARISHAJI | Sami Omary |

tzrailways TRC Reli TV www.trc.co.tz
**Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya**